
# EE BWANA UNISIMAMIE

A Sambaya
Mzumbe university
16.01.2014




**2.Naelewa ya kua wewe ni mwalimu, nguvu zako ni kuu sana, najileta kwako ukanifundishe, niongoze nitimize lengo langu**
**nitakaa na wewe kila siku bwana, nitakua mmoja wako sitaacha kamwe kukutumikia, nakutegemea wewe peke yako**

**3.Najitahidi sana ewe mungu wangu, mda mwingi nawaza sana, nitayawezaje mambo yote haya, naogopa mimi ninahangaika**
**Nafarijika sana nikikukumbuka, mwili wote unafurahi, kwani wewe bwana u pamoja nami, kiongozi tena na mwalimu wangu**

**4.Ahadi yangu bwana ninatoa kwako, siku zote nitakupenda, wewe ndiwe mungu tena kiongozi, nakupenda sana bwana mungu wangu**
**Naomba nijalie matokeo mema,nijalie mafanikio, na nitatangaza neno lako wewe, mataifa waishuhudie kweli**